TANGAZO LA SERIKALI NA.187 la tarehe 17/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA 355)

# AMRI

*(Imetolewa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA LAMAITI YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Lamaiti ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura (355)

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Mji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi.

*Tangazo Serikali Na. 187 (linaendelea)*

______

**JEDWALI**

______

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba LM1 yenye majira - nukta 775848.962MS, 9362187.158KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa kukatiza barabara ya Lamaiti - Ngholi katika uelekeo wa KZ137$^{0}$36''MS kwa umbali wa kilomita 1.34 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba LM2 yenye majira - nukta 776767.270MS, 9361210.129KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS125$^{0}$ kwa umbali wa kilomita 1.35 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba LM3 yenye majira - nukta 776485.991MS, 9359883.848KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KZ68$^{0}$ kwa umbali wa kilomita 0.70 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba LM4 yenye majira - nukta 777184.341MS, 9360010.441KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS144$^{0}$'MS kwa umbali wa kilomita 0.48 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba LM5 yenye majira - nukta 777620.914MS, 9359799.034KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS96$^{0}$ kwa umbali wa kilomita 1.56 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba LM6 yenye majira - nukta 777087.846MS, 9358325.591KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS147$^{0}$'MG kwa umbali wa kilomita 1.78 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba LM7 yenye majira - nukta 775667.934MS, 9357251.546KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS122$^{0}$MG kwa umbali wa kilomita 0.70 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba LM8 yenye majira - nukta 775007.121MS, 9357495.630KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ127$^{0}$MG kwa umbali wa kilomita 3.97 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ya LM9 yenye majira - nukta 773884.280MS, 9361318.920KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KS66$^{0}$MG kwa umbali wa kilomita 2.13 hadi ulipoanzia."

Dodoma
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*